



## TUZO LA MILKEN-MOTSEPE KATIKA TEKNOLOJIA YA KILIMO

### MAPITIO YA PROGRAMU

Taasisi ya Milken na Shirika la Motsepe zimeshirikiana katika mkakati wa miaka mingi kulenga wavumbuzi wa kimataifa na wanabiashara katika kusitawisha masuluhisho yanayoongeza maendeleo yanayoelekeza kufikia Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (United Nations' Sustainable Development Goals (SDGs)). Programu ya Tuzo la Uvumbuzi la Milken-Motsepe ni mfululizo wa mashindano ya tuzo za kiteknolojia yanayotatua baadhi ya matatizo makubwa zaidi duniani—kwa mfano ufikivu wa chakula, nishati, makazi, na elimu—kwa kuangazia bara la Afrika

### TUZO LA MILKEN-MOTSEPE KATIKA TEKNOLOJIA YA KILIMO

Tuzo la kwanza la Milken-Motsepe litaangazia kuongeza maendeleo yanayoelekeza kufikia SDGs 1 na 2: hakuna umasikini na hakuna njaa. Tuzo la Milken-Motsepe Katika Teknolojia ya Kilimo limeundwa ili kuchochea masuluhisho ya uvumbuzi yanayozidisha faida za kiuchumi kwa mashamba madogo na yenye ukubwa wa kiasi kuanzia mbegu hadi mauzo. Usajili ni bure na ni wazi kwa wote, mahali popote, na zawadi kuu la dola milioni moja kwa timu itakayoshinda.

### MPANGILIO WA NYAKATI ZA MASHINDANO NA TUZO

Tuzo la Milken-Motsepe Katika Teknolojia ya Kilimo linajumuisha raundi mbili:

- o Katika **Raundi ya Muundo**, timu zitume muundo na mfumo wao wa biashara. Jopo huru la waamuzi wataalamu watachagua hadi timu 25 zitakazopokea \$10,000 kwa kila timu na kuendelea na mashindano.
- o Katika **Raundi ya Finali**, timu zitaendeleza violezo vyao vya kwanza na kufanya majaribio kwenye mashamba madogo na yenye ukubwa wa kiasi katika Afrika. Waamuzi watatuza zawadi kuu la dola milioni moja, na zawadi zaidi za pesa zitakazogawanywa kati ya mshindi wa pili na watatu, zawadi kwa matumizi bunifu zaidi ya teknolojia za Mapinduzi ya Viwanda ya Nne (4IR), na Zawadi la Chaguo la Watu.

Aprili  
2021

Usajili unafunguliwa

Desemba  
2021

Roundi ya Hati za Muundo

Februari  
2022

Zawadi za Raundi ya Muundo zinatolewa  
Hadi timu 25 zitakazowadiwa  
\$10,000 kwa kila timu

Agosti  
2022

Mkutano wa Timu na  
Maonyesho ya Waekezaji

Aprili  
2023

Zawadi za Raundi ya Muundo zinatolewa  
Zawadi Kuu: Dola Milioni Moja  
Mshindi wa Pili: \$300,000  
Mshindi wa Tatu: \$150,000  
Matumizi Bunifu Zaidi ya 4IR: \$100,000  
Zawadi la Chaguo la Watu: \$100,000

KWA TAARIFA ZAIDI  
Visit [milkenmotsepeprize.org](https://milkenmotsepeprize.org)